**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA**

# TAARIFA YA MAHAFALI YA SABA KWA WAUGUZI NA WAKUNGA

Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania anawataarifu Wahitimu wote wa Kozi ya Uuguzi na Ukunga Waliofaulu Mtihani wa Usajili na leseni uliofanyika tarehe 15/12/2022 kuwa Mahafali ya kutoa vyeti vya Usajili na Leseni yatafanyika siku ya Jumamosi tarehe 18/03/2023 kuanzia saa 1:00 Asubuhi katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete "*Convention*" uliopo njia ya kwenda Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) ikifuatiwa na kilele cha miaka sabini ya Baraza la Uuguzi na Ukunga tarehe **19/03/2023** ambapo Mgeni Rasmi atakuwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

Mada zitakazofundishwa:-
"Lijue Baraza la Uuguzi na Ukunga na kazi zake, Maadili ya Uuguzi na Ukunga, namna ya kuhuisha leseni kwa njia ya kielectroniki pamoja na maswali na majibu yanayohusu Taaluma ya Uuguzi na Ukunga"

Washiriki wote mnatakiwa kuthibitisha Ushiriki wenu kupitia Tovuti ya Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania www.tnmc.go.tz Aidha, mnajulishwa washiriki wote katika mahafali kuvaa Sare ya kitaaluma ***"Professional Uniform"*** iliyoidhinishwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania kama ifuatavyo:-

1) Shati Nyeupe mikono mifupi na Suruali ya Dark Blue kwa Wanaume;
2) Gauni Nyeupe mikono mifupi au Suruali Nyeupe na Blauzi Nyeupe kwa wanawake; na Viatu vya kufunika.

**NB**. **Sandozi au Kandambili haviruhusiwi**.

Kwa mawasiliano piga namba 0784265494, 0655035078 na 0762003800

HMassenga.
Happy Massenga
**KAIMU MSAJILI**

**21/02/2023**

Jengo la Kambarage Tower, Ghorofa ya 5, Barabara ya Benjamini Mkapa, S.L.P 1736, DODOMA Simu: +255262966061/62/63, +255737 962 691, Barua pepe : info@tnmc.go.tz, Tovuti : www.tnmc.go.tz